

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 54 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** AGOSTI 2025

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU MUHIMILI WA UTEKELEZAJI WA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA

2050



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 katika ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete (JKCC) jijini Dodoma tarehe 17 Julai, 2025.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

WALIMU NA DIRA YA TAIFA 2050 - WAKATI WA KUCHUKUA HATUA NI SASA


Tanzania inapoanza kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, macho yote yanaelekezwa kwenye sekta ya elimu kama mhimili wa mafanikio ya muda mrefu. Katika dira hiyo, elimu bora imeainishwa kuwa msingi wa kuifikisha nchi kwenye uchumi wa kati wa juu unaoongozwa na maarifa, teknolojia na ubunifu. Ndani ya mfumo huo, hakuna mhusika muhimu kama mwalimu. Walimu ndio wanaoweka msingi wa maarifa, ujuzi na maadili kwa kizazi kijacho ambacho ndicho kitakachotimiza malengo ya taifa.

Kwa kutambua umuhimu huo, Tume ya Utumishi wa Walimu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia utumishi wa walimu kikamilifu kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura ya 448 kwa kuhakikisha walimu wanatekeleza majukumu yao kwa amani na utulifu huku maadili ya kazi yakiwa yanazingatiwa.

Dira ya Taifa haiwezi kuwa halisi iwapo walimu wataona kazi yao kama ajira ya kawaida tu. Walimu wanapaswa kutambua kuwa wao ni wabeba ndoto ya taifa. Wanapaswa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anayepitia mikononi mwao ni mzalendo wa kesho, mtaalamu wa kesho, au kiongozi wa kesho. Hivyo basi, kila somo lina thamani ya taifa, kila kauli yenye motisha ni uwekezaji katika mustakabali wa nchi, na kila nidhamu wanayoonyesha ni kiashiria cha jamii tunayotaka kuijenga. Walimu wanapaswa kuwa mstari wa mbele si tu katika kufundisha, bali pia katika kuwa mfano wa maadili, nidhamu na uzalendo kwa taifa.

Wito wetu kwa walimu nchini ni huu: endeleeni kufanya kazi kwa moyo, kwa weledi na kwa maadili. Taifa linawaamini. Tume ya Utumishi wa Walimu inawaamini na itaendeleza jitihada zake katika kusimamia masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu ili kufikia malengo ya Dira yetu.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz

Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, S.L.P 353, DODOMA.



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU MUHIMILI WA UTEKELEZAJI WA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2050

Na Mwandishi Wetu, Dodoma.

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, iliyozinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan hivi karibuni, inalenga kujenga Tanzania kuwa taifa lenye uchumi wa kati wa juu unaoongozwa na watu wake walioboea katika elimu, ubunifu, maarifa na teknolojia.

Katika safari hii ya mageuzi ya kimumo na kiuchumi, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inabeba jukumu muhimu katika kuhakikisha kuwa sekta ya elimu inakuwa injini ya mabadiliko hayo yanayotarajiwa kuifikisha Tanzania kwenye hatua mpya ya maendeleo.

Rais Samia, katika uzinduzi wa Dira hiyo, alieleza bayana kuwa mafanikio ya dira hayawezi kufikiwa bila uwekezaji wa dhati katika rasilimali watu, hasa kupitia elimu bora, maadili mema, na usawa wa kijinsia.

Alisisitiza kuwa walimu ni uti wa mgongo wa mfumo wa elimu, na hivyo ni lazima kuwekwa katika mazingira bora ya kazi, kupewa mafunzo ya mara kwa mara, na kuwezesha ili waweze kuwajengea wanafunzi maarifa, ujuzi na maadili yanayohitajika katika dunia ya sasa.

Kauli hiyo imekuwa dira ya pili kwa taasisi kama Tume ya Utumishi wa Walimu, ambayo imekuwa ikijipanga kuhakikisha kwamba walimu wanakuwa chachu ya mageuzi ya elimu kwa vitendo.

TSC, kama chombo cha kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu, imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa elimu inatolewa na walimu wenye sifa, weledi, ufanisi na maadili yanayokubalika.

Kupitia matumizi ya mifumo ya kidijitali kama TSCMIS (Teachers' Service Commission Management Information System), Tume imefanikiwa kuboresha huduma kwa walimu katika maeneo ya ajira,



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akionesha nakala za vitabu vya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 mara baada ya uzinduzi katika ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete (JKCC) jijini Dodoma tarehe 17 Julai, 2025.

kupandishwa vyeo, kubalilishiwa kazi/cheo na masuala mengine ya kiutumishi, jambo linalosaidia kuongeza uwazi, ufanisi na motisha kwa walimu kote nchini.

Mbali na hayo, Tume imeendelea kuhakikisha mpango wa mafunzo kwa walimu unazingatiwa ili walimu wapate fursa ya kujiendeleza kielimu kwa kuzingatia sheria, Kanuni na Taratibu za kiutumishi. Vilevile, Tume imejipanga kuendelea kutoa elimu kwa walimu pale wanapoamua kujiendeleza ili kuleta manufaa kwao binafsi na kuboresha utendaji wao wa kazi.

Katika kuimarisha usawa na maendeleo jumuiishi, Tume ina jukumu la kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa Walimu ndani ya Serikali za Mitaa na Shule, ili kila mtoto wa Kitanzania apate fursa sawa ya kupata elimu bora bila kujali alipo.

Aidha, TSC imekuwa mstari wa mbele kusimamia nidhamu ya walimu, kwa kuhakikisha wanafuata maadili ya kazi na kuwajibika ipasavyo. Hatua hii imeongeza

uadilifu, imani ya jamii kwa walimu na kuimarisha hadhi ya taaluma ya ualimu nchini.

Mchango wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 hauishii tu katika masuala ya kiutawala bali unagusa moja kwa moja msingi wa mafanikio ya muda mrefu ya taifa.

Walimu wanaosimamiwa na Tume ndio wanaotegemewa kuwajenge watoto wa leo kuwa viongozi, wataalamu, wajasiriamali na raia bora wa kesho. Kupitia kazi yao, ndoto ya kuwa na Tanzania yenye uchumi wa kati wa juu, unaotegemea maarifa na teknolojia, inapata msingi imara wa utekelezaji.

Dira ya 2050 si ndoto ya mbali, bali ni mwito wa sasa wa kuchukua hatua madhubuti. Tume ya Utumishi wa Walimu ikiwa na dhamana ya kusimamia utumishi wa walimu, imejipanga kuendelea kuwa mshirika wa karibu katika safari hii ya kitaifa ya mageuzi ya kweli, yenye lengo la kuibadilisha Tanzania kuwa taifa la kisasa, lenye usawa na maendeleo kwa wote.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU MUHIMILI WA UTEKELEZAJI WA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2050



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akigawa nakala ya kitabu cha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango baada ya kuzindua Dira hiyo ya Taifa ya Maendeleo 2050 katika ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete (JKCC) jijini Dodoma tarehe 17 Julai, 2025.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akigawa nakala ya kitabu cha Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi baada ya kuzindua Dira hiyo ya Taifa ya Maendeleo 2050 katika ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete (JKCC) jijini Dodoma tarehe 17 Julai, 2025.



TSC YAENDELEA KUIMARISHA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA WALIMU KWA BAJETI YA BILIONI 21.85

Na Mwandishi Wetu - Dodoma

Mwishoni mwa mwezi Juni, 2025 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha bajeti ya Serikali ya shilingi trilioni 56.49 kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ilitengewa shilingi bilioni 21.85 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya kusimamia masuala ya utumishi wa walimu nchini.

Katika bajeti hiyo ya Tume, shilingi bilioni 19.90 zitatumika kwa Matumizi ya Kawaida, ikiwa ni pamoja na shilingi bilioni 11.79 kwa mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 8.11 kwa matumizi mengineyo kama vile kushughulikia maadili na nidhamu, upandishaji wa vyeo, recategorization, pamoja na elimu kwa walimu kuhusu haki na wajibu wao katika utumishi wa umma.

Aidha, Tume imepata shilingi bilioni 1.94 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ambapo shilingi bilioni 1.68 ni fedha za nje kutoka kwa wahisani na shilingi milioni 264.22 ni fedha za ndani. Miradi hiyo inalenga kuboresha mifumo ya TEHAMA, kuongeza uwazi na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu.

Akizungumza baada ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo,



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke, alisema kuwa fedha hizo ni sehemu ya mkakati mpana wa serikali wa kuimarisha rasilimali watu katika sekta ya elimu, kupitia usimamizi bora wa walimu watumishi wa umma waliopo shuleni.

"Kupitia bajeti hii, Tume itaongeza kasi ya kushughulikia masuala ya walimu kwa haki na kwa wakati. Tunalenga kuimarisha nidhamu, uwajibikaji, na kuboresha huduma za kiutumishi ili kuinua morali ya

walimu," alisema Prof. Muruke.

Kwa upande wake, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, alieleza kuwa kupitishwa kwa bajeti hiyo ni matokeo ya dhamira njema ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuboresha sekta ya elimu nchini.

"Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa moyo wake wa dhati katika kuimarisha sekta ya elimu. Uwekezaji huu unachochea upatikanaji wa rasilimali fedha kwa taasisi kama TSC ili ziweze kutimiza majukumu yao kwa ufanisi," alisema Mwl. Nkwama.

Bajeti ya Tume inajibu kwa vitendo malengo ya Bajeti Kuu ya Serikali ya 2025/26 ambayo imesisitiza kuimarisha huduma za kijamii, hasa elimu na afya, huku serikali ikielekeza rasilimali nyingi katika kuboresha mazingira ya utoaji huduma kwa wananchi.

Kwa upande wa sekta ya elimu, serikali imesisitiza kuwa ubora wa elimu hauwezi kufikiwa bila kuwekeza katika usimamizi madhubuti wa walimu – jambo ambalo linafanywa na TSC. Hivyo, uwezesaji wa Tume kupitia bajeti hii ni hatua ya msingi kuelekea utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MAONESHU YA NANENANE KITAIFA – TSC YAWA KIVUTIO KWA KUTOA HUDUMA BORA

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, ameongoza hafla ya uzinduzi rasmi wa Maonesho ya Wakulima ya Nanenane Kitaifa yaliyofanyika tarehe 1 Agosti 2025 katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Maonesho ya mwaka huu yanachagizwa na kauli mbiu: “Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi” na yanatarajiwa kufikia kilele chake tarehe 8 Agosti, 2025.

Akihutubia maelfu ya wananchi na washiriki wa maonesho hayo, Dkt. Mpango aliipongeza Kamati ya Maandalizi kwa kuandaa maonesho yaliyobeba sura ya kitaifa na kueleza kuwa sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi ni nguzo kuu ya uchumi wa Taifa. Alibainisha kuwa sekta hizo zimechangia ajira kwa Watanzania

na kuiingizia nchi zaidi ya shilingi bilioni 3.4 za fedha za kigeni.

Dkt. Mpango alisema kuwa Tanzania kwa sasa inajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 128, hali inayoashiria mafanikio ya sera na mikakati ya serikali katika sekta ya kilimo. Aidha, alieleza kuwa Serikali imeongeza bajeti ya sekta hizo hadi kufikia shilingi trilioni moja, ikiwa ni mkakati wa kuimarisha uzalishaji, kuendeleza tafiti za mbegu bora, na kuboresha miundombinu ya uzalishaji na masoko.

Aidha, Dkt. Mpango ametoa wito kwa wananchi kushiriki kwa amani uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2025 na kuwataka watembelee mabanda ya maonesho ili kujifunza teknolojia na mbinu mpya za kisasa za kilimo, mifugo na uvuvi.

TSC YAWA KIVUTIO KWA KUTOA HUDUMA NANENANE

Miongoni mwa taasisi zilizovutia watu wengi katika maonesho hayo ni Tume ya Utumishi wa Walimu

(TSC), ambayo imeweka banda lake katika viwanja vya Nzuguni na kutoa huduma mbalimbali kwa walimu na wananchi wanaofika kwenye maonesho hayo.

Katibu wa Tume hiyo, Mwalimu Paulina Nkwama, ameongoza kwa mfano kwa kutoa huduma moja kwa moja kwa wananchi, ikiwa ni ishara ya kujituma na kusogeza huduma karibu na walengwa.

Huduma zinazotolewa na Tume katika banda lake ni pamoja na kutoa elimu kuhusu masuala ya ajira, Maadili na Maendeleo ya walimu.

Banda la TSC limekuwa kivutio kwa wageni wengi, likisisitiza misingi ya uwajibikaji, uwazi na utoaji wa huduma bora, sambamba na kuchangia katika uboreshaji wa sekta ya elimu nchini.

Ushirikiwa Tume katika maonesho haya unaonesha dhamira ya Serikali katika kuboresha elimu sambamba na kukuza sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akihutubia wakati wa ufunguzi wa maonesho ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma, tarehe 01 Agosti 2025.

MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MAONESHU YA NANENANE KITAIFA – TSC YAWA KIVUTIO KWA KUTOA HUDUMA BORA



Viongozi mbalimbali waliohudhuria hafla ya ufunguzi wa maonesho ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma, tarehe 01 Agosti 2025.



Baadhi ya washiriki waliohudhuria hafla ya ufunguzi wa maonesho ya Nanenane Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni Jijini Dodoma, tarehe 01 Agosti, 2025 wakiwa katika hali ya utulivu.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akitoa huduma kwa mteja katika banda la TSC kwenye Maonesho ya Wakulima (Nane Nane) kitaifa jijini Dodoma.

MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MAONESHU YA NANENANE KITAIFA – TSC YAWA KIVUTIO KWA KUTOA HUDUMA BORA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akitoa huduma kwa wateja waliofika kwenye banda la TSC katika Maonesho ya Wakulima (Nane Nane) kitaifa jijini Dodoma.



Huduma zikiendelea kutolewa katika banda la TSC wakati wa maonesho ya Nanenane kitaifa jijini Dodoma.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

88
2025

KARIBU HUKU KUMENOGA



Wateja mbalimbali wakipata huduma kwenye banda la Tume ya Utumishi wa Walimu.

"Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi."



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

88
2025

KARIBU HUKU KUMENOGA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akiendelea kutoa huduma kwa mteja katika banda la TSC kwenye Maonesho ya Wakulima (Nane Nane) yanayofanyika kitaifa jijini Dodoma. Maadhimisho ya mwaka huu yalianza rasmi tarehe 1 Agosti 2025 na yatafikia kilele chake tarehe 8 Agosti 2025. Banda la TSC limeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa walimu na wananchi, likisisitiza uwajibikaji, uwazi na utoaji wa huduma bora kwa walimu kote nchini.

Kauli mbiu: "Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi."



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

88
2025

KARIBU HUKU KUMENOGA



***Wateja mbalimbali wikipata huduma kwenye
banda la Tume ya Utumishi wa Walimu.***

"Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi."



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

TSC YABAINISHA MAFANIKIO YA MPANGO MKAKATI WAKE 2021/22 – 2025/26, YAWEKA MWELEKEO MPYA KUELEKEA MWAKA 2031

Na Mwandishi Wetu – Singida.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wake wa miaka mitano kwa mafanikio makubwa, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa dira na mipango ya maendeleo ya Taifa. Hadi sasa, Mpango Mkakati wa pili wa Tume (2021/22 – 2025/26) umewezesha kuboreshwa kwa huduma kwa walimu na wadau mbalimbali katika sekta ya elimu.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa Kikao Kazi cha Mapitio ya Mpango Mkakati huo katika Ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, mkoani Singida, Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama alisema mapitio hayo ni maandalizi ya mpango mpya wa miaka mitano kuanzia mwaka 2026/27 – 2030/31.

Katika kipindi cha utekelezaji wa mpango wa sasa, mafanikio makubwa yameripotiwa. Mwalimu Nkwama alieleza kuwa jumla ya walimu 67,352 wameajiriwa na kusajiliwa, 10,131 walithibitishwa kazini, na 545,395 walipandishwa

vyeo. Aidha, walimu 4,357 walibadilishiwa cheo au kazi baada ya kujiendeleza, na 8,726 walipatiwa vibali vya kustaafu. Vilevile, Tume ilipokea na kushughulikia majalada 65 ya madai ya walimu kuhusu mafao ya pensheni, mirathi na mikataba.

Katika kuimarisha weledi wa watumishi wake, Tume imetoa mafunzo elekezi kwa walimu wapya kupitia mfumo wa “Training of Trainers (ToT)”. Mafunzo hayo yamewafikia makatibu wasaidizi wa wilaya 139, watumishi wa Tume 508, makamishna 10, wajumbe wa kamati za wilaya 139, na maafisa elimu wa wilaya 139. Pia mashauri ya walimu 4,930 yalithitimishwa na rufaa 327 kuamuliwa.

Mwalimu Nkwama alibainisha kuwa Tume imekamilisha kazi ya kufungamanisha mifumo ya TEHAMA ya TSCMIS, SIS, e-Watumishi na TPPS ili kurahisisha uendesaji wa masuala ya nidhamu na rufaa kwa walimu. Vilevile, Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapya umeandaliwa na kusambazwa kwa walimu 14,648. Aidha, mwongozo

wa masuala ya nidhamu na rufaa nao umetolewa kwa ajili ya kuwajengea uwezo watendaji wa Tume.

Akielezea historia ya mikakati hiyo, Katibu huyo alisema kuwa Mpango Mkakati wa kwanza wa Tume ulitekelezwa kati ya mwaka 2016/17 hadi 2020/21 na kufuatiwa na mpango wa sasa ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka wa fedha 2025/26.

Mwl. Nkwama alisisitiza kuwa kufanya mapitio ya Mpango Mkakati ni muhimu ili kuhakikisha Tume inabaki kwenye mwelekeo wa kutimiza majukumu yake kikamilifu, kujitathmini katika maeneo ya utendaji, na kufanya maamuzi sahihi kwa kutumia takwimu. Pia alisema kuwa hatua hiyo itawezesha Tume kuendelea kutoa huduma bora kwa walimu nchini.

Aliwataka washiriki wote wa kikao hicho kuhakikisha wanazingatia kwa makini maelekezo ya wawezeshaji wao ili matokeo ya mapitio hayo yachangie kuandaa mpango wenye tija kwa maendeleo ya Tume na sekta ya elimu kwa ujumla.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama.

TSC IRINGA YAIPONGEZA SERIKALI KWA UTATUZI WA KERO ZA WALIMU



Bi. Frida N. Mwiwula, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Iringa, akiendelea na majukumu yake.

Na Mwandishi Wetu – Iringa

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Iringa imeipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada zake za dhati katika kushughulikia changamoto na kero zilizokuwa zikiwakabili walimu nchini.

Akizungumza hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Iringa, Bi. Frida Mwiwula, alisema kuwa hatua zilizochukuliwa na Serikali kupitia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, zimeleta faraja kubwa kwa walimu.

“Rais ameturahisishia kazi kwa kujibu hoja za walimu kuhusu kupunjwa madaraja. Baada ya msawazo kufanyika na walimu kupata madaraja yao, wengi wamefurahi na kuacha kuja ofisini kudai haki zao. Wanasema ‘Mama ameupiga mwingi’ na wanapendekeza aongezewe miaka mingine kumi kwa maslahi ya walimu,” alisema Bi. Mwiwula.

Alibainisha kuwa utatuzi wa kero unafanyika kwa wakati, hali inayowezesha kila mhusika kuwajibika ipasavyo katika nafasi yake, na hivyo kupunguza

malalamiko.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 hadi 2024/25, jumla ya walimu 2,739 kutoka Wilaya ya Iringa wamepandishwa vyeo, wakiwemo walimu 1,630 wa shule za msingi na 1,109 wa shule za sekondari.

Mwalimu Mary Abel Moshiro kutoka Shule ya Msingi Kibwabwa alisema:

“Kwa kweli Mama ni Mama. Aendelee kutuongoza, kwani ametufanyia mengi. Tumepandishwa madaraja kwa wakati, na miundo ya utumishi imeboreshwa.”

Naye Mwalimu Yovita Laurent Makoi kutoka shule hiyo hiyo aliongeza kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa ya kuboresha miundombinu ya shule na kutatua kero za walimu.

“Malalamiko yetu yamesikilizwa, na walimu tunaendelea kuneemeka na uongozi huu,” alisema.



Maafisa wa TSC Wilaya ya Iringa; kutoka kushoto: Bw. Lufingo E. Mng'ong'o (Afisa Nidhamu na Maadili ya Walimu), Bi. Frida N. Mwiwula (Kaimu Katibu Msaidizi), na Bi. Agness E. Makupa (Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu).

TSC IRINGA YAIPONGEZA SERIKALI KWA UTATUZI WA KERO ZA WALIMU



Bw. Lufingo E. Mng'ong'o akifafanua kuhusu nidhamu na maadili ya walimu katika kikao cha tathmini ya matokeo, Manispaa ya Iringa.



Bw. Lufingo E. Mng'ong'o akitoa mada kuhusu maadili ya utumishi wa umma kwa wakuu wa shule na Maafisa Elimu Kata, Manispaa ya Iringa.



TSC KIBONDO YATOA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WA AJIRA MPYA

Na Mwandishi Wetu – Kibondo

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibondo imeendesha mafunzo elekezi kwa walimu wapya walioajiriwa mwaka 2025 ili kuwaandaa rasmi kwa majukumu yao katika utumishi wa umma.

Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 4 Julai 2025 katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, yakihudhuriwa na washiriki 67 kutoka shule mbalimbali wilayani humo.

Mgeni rasmi katika ufunguzi wa mafunzo hayo alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wilaya ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Hussein Mondo, ambaye alifungua rasmi mafunzo hayo majira ya saa 3:30 asubuhi.

Akizungumza wakati wa ufunguzi, Mwl. Mondo aliwataka walimu wapya kuwa mfano wa kuigwa katika jamii kwa kudumisha maadili, uadilifu na uzalendo, huku wakitekeleza wajibu wao kwa weledi na kufuata sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Mafunzo hayo yaliendeshwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Kibondo, Mwl. Mawazo I. Abely, pamoja na Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu, Bw. Julius Bugagi.

Viongozi hao waliwasilisha mada mbalimbali zikiwemo Sheria za Utumishi wa Walimu, Haki na Wajibu wa Mwalimu, Taratibu za Ajira, Maadili ya Utumishi wa Umma, pamoja na namna ya kushughulikia changamoto za kitaaluma na kiutumishi shuleni.

Mada hizo zililenga kuwajengea walimu uelewa mpana kuhusu mfumo wa ajira serikalini, nafasi yao kama watumishi wa umma, pamoja na jinsi ya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi bila kuvunja maadili ya kazi.

Aidha, Katibu wa Chama cha Walimu Wilaya ya Kibondo, Mwl. Mbwambo, alihudhuria pia mafunzo hayo na kutoa salamu za chama, akiwahimiza walimu kujiunga na CWT na kushiriki katika shughuli za maendeleo ya walimu kijumla.



Picha mbalimbali za washiriki wa mafunzo elekezi kwa walimu wapya walioajiriwa mwaka 2025 katika Wilaya ya Kibondo.

Mafunzo hayo ni sehemu ya mkakati wa TSC kuhakikisha kila mwalimu mpya anaanza kazi akiwa na maarifa ya msingi ya kisheria, kitaaluma na kiutumishi, ili kuepusha changamoto zinazotokana na kutokujua haki na wajibu kazini.

“Ni matumaini yetu kuwa mafunzo haya yatawawezesha walimu wapya

kutekeleza majukumu yao kwa weledi, ufanisi na nidhamu ya hali ya juu,” alisema mmoja wa wawezeshaji.

Walimu walioshiriki waliipongeza Tume kwa kuandaa mafunzo hayo muhimu kabla ya kuanza kazi rasmi, wakisema yamewajengea uelewa na kuwapa mwongozo sahihi wa kuanza safari yao katika taaluma ya ualimu.

TSC KIBONDO YATOA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WA AJIRA MPYA



Picha mbalimbali za washiriki wa mafunzo elekezi kwa walimu wapya walioajiriwa mwaka 2025 katika Wilaya ya Kibondo.

TSC MUFINDI YAFANYA ZIARA KUELIMISHA WALIMU KUHUSU KUZINGATIA SHERIA NA MAADILI YA KAZI

Na Mwandishi Wetu – TSC Mufindi

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mufindi imefanya ziara ya kikazi katika shule mbalimbali wilayani humo kwa lengo la kutoa elimu kuhusu kanuni za maadili na utendaji kazi katika taaluma ya ualimu.

Akizungumza wakati wa mahojiano maalum na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Tume, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mufindi, Bi. Leonia Lucas Nduye, alisema kuwa ziara hiyo ilihusisha Shule za Sekondari za Idunda, Sao Hill, Ihowanza, Kibengu na Shule za Msingi za Kiponda na Idumulavanu.

Alieleza kuwa katika utekelezaji wa zoezi hilo, Maafisa wa Tume walitumia mbinu mbalimbali ikiwemo vikao na wakuu wa shule, Maafisa Elimu Kata na wadau wa elimu, utoaji wa ushauri nasaha kwa walimu wenye changamoto, matumizi ya matini mbalimbali na vipeperushi.

Katika hatua nyingine, Bi. Leonia aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kushughulikia kero za walimu wilayani humo. Alifafanua kuwa katika kipindi cha uongozi wa Serikali hiyo, jumla ya walimu 1,778 walipandishwa vyeo — wakiwemo walimu 1,013 wa shule za msingi na 765 wa shule za sekondari.

Aidha, alieleza kuwa Serikali imekuwa ikijitahidi kulipa madeni ya walimu kwa kadri fedha zinavyotolewa, hatua ambayo imeleta matumaini makubwa kwa walimu. Bi. Leonia aliongeza kuwa jitihada hizo zimekwenda sambamba na nyongeza ya mishahara, uboreshaji wa mtaala wa elimu ikiwemo elimu ya awali, na kuimarisha maslahi ya walimu kwa ujumla.

Akizungumzia suala la nidhamu na maadili kazini, Bi. Leonia alieleza kuwa mafunzo yaliyotolewa kwa wajumbe wa kamati za nidhamu na wakuu wa shule yameleta mabadiliko chanya. Alisema kuwa mafunzo hayo yamewajengea uelewa mpana



Bi. Leonia Lucas Nduye, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mufindi akiwa ofisini kwake.

kuhusu sheria, kanuni na maadili ya kazi ya ualimu, hivyo kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi kwa mujibu wa sheria.

“Mafunzo haya yameongeza nidhamu na maadili miongoni mwa walimu. Wakuu wa shule sasa wanatambuliwa kama mamlaka za

nidhamu, na wameweza kuchagua aina sahihi ya adhabu kwa walimu wanaokiuka taratibu,” alisema.

Alibainisha kuwa walimu waliopata elimu hiyo wamekuwa mabalozi katika maeneo yao ya kazi kwa kuelimisha wenzao kuhusu wajibu na taratibu za kiutumishi.

TSC MUFINDI YAFANYA ZIARA KUELIMISHA WALIMU KUHUSU KUZINGATIA SHERIA NA MAADILI YA KAZI



Maafisa wa TSC Wilaya ya Mufindi katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Sekondari Kibengu baada ya kutoa elimu kuhusu maadili na utendaji kazi.



Maafisa wa TSC wakiwa katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Msingi Idumulavanu baada ya kutoa elimu.



Bi. Leonia Lucas Nduye (kulia) akitoa huduma kwa Mwalimu Cresensia Paul Mgao (kushoto) aliyepandishwa daraja kwa mserekeo.



Maafisa wa TSC wakiwa katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Msingi Idumulavanu baada ya kutoa elimu.



Maafisa wa TSC wakiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibengu baada ya kutoa elimu juu ya maadili ya kazi ya ualimu.

Picha za Matukio mbalimbali wakati Kikao cha Kamati ya Ukaguzi ya Tume ya Utumishi wa Walimu kikiwa kinaendelea. Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni jijini Dodoma.



TSC WILAYA YA RUFJI YAWAPIGA MSASA WALIMU WA AJIRA MPYA

Na Mwandishi Wetu – Rufiji

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rufiji imetoa mafunzo elekezi kwa walimu wapya walioajiriwa mwaka 2025 kwa lengo la kuwawezesha kuanza kazi wakiwa na uelewa wa sheria, taratibu na misingi ya maadili ya utumishi wa umma.

Mafunzo hayo yalifanyika tarehe 3 Julai 2025 katika shule ya sekondari Ikwiriri, yakilenga kuwaandaa walimu kutoa huduma bora inayozingatia maadili ya kiutumishi.

Jumla ya walimu 37 waliopangwa awamu ya kwanza walihudhuria mafunzo hayo ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa mwongozo wa kitaifa ulioandaliwa na TSC Makao Makuu, ambao unasisitiza umuhimu wa mafunzo elekezi kwa kila mwalimu anayeajiriwa kabla ya kuanza rasmi majukumu ya kufundisha.

Mafunzo hayo yalijumuisha mada muhimu ikiwemo: Sheria na Taratibu za Utumishi wa Umma, Maadili ya Kitaaluma, Haki na Wajibu wa Mwalimu, pamoja na taratibu za ajira na maendeleo ya kiutumishi. Washiriki walijifunza kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma (Sura 298), Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, na Sheria ya TSC (Sura 448) pamoja na kanuni zake za mwaka 2016.

Katika mada ya maadili na nidhamu, walimu walielekezwa namna ya kujiepusha na vitendo vinavyokiuka maadili ya kazi, kutambua taratibu za kushughulikia malalamiko na namna bora ya kuwajibika kwa jamii inayowazunguka.

Walimu waliopata mafunzo walieleza kuwa yamewajengea ujasiri, uelewa na mwelekeo wa kazi, huku wakiahidi kutekeleza majukumu yao kwa bidii na uadilifu.



Picha mbalimbali za washiriki wa mafunzo ya walimu wa Ajira mpya katika Wilaya ya Rufiji.

TSC WILAYA YA RUFJI YAWAPIGA MSASA WALIMU WA AJIRA MPYA



Picha mbalimbali za washiriki wa mafunzo ya walimu wa Ajira mpya katika Wilaya ya Rufiji.

MAAFISA HABARI SERIKALINI WAJENGWA UWEZO KUTANGAZA MAFANIKIO YA PROGRAMU YA SHULE BORA

Na Mwandishi Wetu – Korogwe

Katika juhudi za kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu utekelezaji wa miradi ya elimu nchini, Maafisa Habari kutoka Wizara, Taasisi na Mikoa inayotekeleza programu ya Shule Bora wamejengwa uwezo maalum wa kimkakati kupitia warsha ya siku tano iliyoandaliwa chini ya Programu hiyo.

Warsha hiyo, iliyofanyika katika Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, ililenga kuwawezesha Maafisa Habari kubeba jukumu muhimu la kuibua, kuandaa, na kusambaza taarifa zenye mvuto kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita, hususan katika maboresho ya sekta ya elimu ya msingi.

Akifungua rasmi mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Bi. Amina Kibunde, alisisitiza kuwa jukumu la mawasiliano serikalini limekuwa la kimkakati zaidi, hivyo linahitaji maarifa mapya, ubunifu, na matumizi ya mbinu za kisasa ili kuvuta usikivu wa jamii.

“Maafisa Habari si waandishi tu wa taarifa; ni mashujaa wa mabadiliko. Kupitia maneno yao, miradi ya Serikali inapata uhai kwa wananchi,” alisema Bi. Amina huku akisisitiza matumizi ya majukwaa yote ya



Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Bi. Amina Kibunde akifungua Warsha ya Maafisa Habari iliofanyika hivi karibuni mjini Korogwe.

mawasiliano, ikiwemo mitandao ya kijamii, redio, na televisheni kufikisha ujumbe chanya wa maendeleo.

Warsha hiyo imewakutanisha Maafisa Habari kutoka TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), pamoja na Maafisa kutoka taasisi za elimu washirika wa Shule Bora, kutoka mikoa tisa: Dodoma, Simiyu, Mara, Singida, Kigoma, Katavi, Rukwa, Tanga na Pwani.

Kwa upande wake, Kiongozi wa Timu ya Shule Bora, Bi. Virginie Briand, alisema kuwa Programu ya Shule Bora inatekelezwa kwa lengo la kuweka misingi imara ya utoaji wa elimu bora kwa kila mtoto. Mafunzo haya ni sehemu ya mkakati wa kuhakikisha mafanikio hayo hayaishii kimya kimya, bali yanawafikia wananchi kwa lugha rahisi na yenye msisimko.

Katika siku ya kwanza ya mafunzo, washiriki walifundishwa namna ya kuandaa mikakati madhubuti ya mawasiliano, mbinu za uandishi wa taarifa zenye mvuto kwa jamii, na misingi ya ushawishi kwa kutumia takwimu na ushuhuda halisi wa walimu, wazazi na wanafunzi.

Miongoni mwa washiriki kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu, walikiri kuwa mafunzo hayo yamefungua ukurasa mpya wa namna wanavyoweza kuonyesha matokeo ya kazi zao kwa njia inayoeleweka na kupokelewa vyema na jamii.

Katika zama ambazo taarifa hupatikana kwa kasi, na wakati mwingine huchanganyika na upotoshaji, Serikali kupitia mafunzo haya inajenga ngome imara ya mawasiliano ya maendeleo – ikihakikisha kwamba mafanikio ya kila sarafu ya umma yanatajwa, yanaonekana, na yanatambulika.



Baadhi ya washiriki wa Warsha ya Maafisa Habari iliofanyika hivi karibuni mjini Korogwe wakiendelea na mafunzo.

MAAFISA HABARI SERIKALINI WAJENGWA UWEZO KUTANGAZA MAFANIKIO YA PROGRAMU YA SHULE BORA



Baadhi ya washirikiwa wa Warsha ya Maafisa Habari iliofanyika hivi karibuni mjini Korogwe wakiendelea na mafunzo.



Kiongozi wa Timu ya Shule Bora, Bi. Virginie Briand akitoa amelezo ya utangulizi wakati wa ufunguzi wa warsha hiyo iliyofanyika hivi karibuni mjini Korogwe.



Picha ya pamoja ya washiriki wa Warsha ya Maafisa Habari iliofanyika hivi karibuni mjini Korogwe.



Washiriki wa Warsha ya Maafisa Habari iliofanyika hivi karibuni mjini Korogwe wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa mafunzo.

WALIMU WAPYA KINONDONI WAELIMISHWA JUU YA HAKI, WAJIBU NA MAADILI YA UTUMISHI WA UMMA

**Na Mwandishi Wetu –
Dar es Salaam**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kupitia Ofisi yake ya Wilaya ya Kinondoni imeendesha mafunzo elekezi kwa walimu wapya walioajiriwa mwaka 2025, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuwaandaa kitaaluma na kuwajengea uelewa juu ya majukumu yao katika utumishi wa umma.

Mafunzo hayo yaliyofanyika tarehe 4 Julai 2025, yaliwaleta pamoja walimu 95 waliopangiwa shule mbalimbali za msingi na sekondari katika Manispaa ya Kinondoni.

Kwa mujibu wa taarifa ya Tume, lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwajengea walimu hao uelewa kuhusu historia, muundo na majukumu ya TSC, pamoja na sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia Utumishi wa Walimu na wa Umma kwa ujumla.

Miongoni mwa mada zilizowasilishwa ni pamoja na: historia ya Tume ya Utumishi wa Walimu, taratibu za ajira na maendeleo ya walimu, haki na wajibu wa walimu, maadili na nidhamu, pamoja na taratibu za mawasiliano serikalini na namna ya kushughulikia malalamiko kazini.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kinondoni, Bw. Theobald Kilindo aliweka wazi kuwa walimu wanapaswa kuelewa na kuzingatia sheria ya Utumishi wa Umma (Sura 298), Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu (Sura 448), pamoja na taratibu mbalimbali zinazowaongoza katika utendaji kazi wao wa kila siku.

Aidha, walimu walifahamishwa juu ya stahiki zao kama likizo, mafunzo kazini, posho mbalimbali,



Picha mbalimbali za washiriki wa mafunzo ya walimu wa ajira mpya katika Wilaya ya Kinondoni yaliyofanyika hivi karibuni.

huduma za afya, fidia, pamoja na haki ya kushiriki shughuli za kisiasa kwa mujibu wa sheria.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni pia alipata fursa ya kuzungumza na walimu hao, ambapo alijibu hoja na maswali mbalimbali yaliyowasilishwa na walimu wa ajira mpya, huku akiwataka kuwa waadilifu na mfano

wa kuigwa katika jamii.

Walimu hao walionyesha shukrani kwa Tume kwa kuwaandalia mafunzo hayo, wakieleza kuwa yamewapa mwanga mkubwa juu ya wajibu wao kama watumishi wa umma. Waliahidi kuzingatia misingi ya sheria, kanuni na maadili ya taaluma yao.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu